# HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA SHINYANGA MHESHIMIWA ZAINAB R. TELACK WAKATI WA UZINDUZI WA BODI YA USHAURI YA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA SHINYANGA ULIOFANYIKA KWENYE UKUMBI MKUBWA WA MIKUTANO WA OFISI YA MKUU WA MKOA TAREHE 17 MEI, 2017

***Katibu Tawala wa Mkoa,***

***Katibu Tawala msaidizi Sehemu ya Afya (Mganga Mkuu wa Mkoa),***

***Mwenyekiti wa Bodi teule, Dkt Ernest Haraka***

***Ndugu wajumbe wote wa bodi,***

***Wataalam Mbalimbali mlioko mahali hapa,***

***Mabibi na Mabwana,***

***Habari za Asubuhi.***

***Ndugu Wajumbe,***

Awali ya yote ninapenda kumshukuru mwenyezi mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutujalia sisi sote afya njema na kutufanya tuweze kukutana siku hii ya leo.

Kwa namna ya pekee, natoa shukrani zangu za dhati kwa uongozi wa Hospitali ya Mkoa chini ya Katibu Tawala wa Mkoa kwa kunialika kuwa Mgeni rasmi  kwenye shughuli hii adhimu ya kuzindua bodi ya ushauri ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga.

***Ndugu Wajumbe,***

Bodi ya ushauri ya hospitali ya rufaa ya Mkoa ni chombo muhimu sana katika uendeshaji wa huduma za afya za hospitali za mikoa. Hiki ndicho chombo pekee kinacho waunganisha wananchi na serikali yao katika ngazi ya hospitali ya rufaa ya Mkoa. Ni chombo ambacho kina wawakilisha wananchi katika kufanya maamuzi juu ya utoaji wa huduma katika hospitali ya rufaa ya Mkoa. Bodi inaweza kufananishwa na kioo ambacho menejimenti ya hospitali inakitumia kupata mrejesho wa namna wanavyotoa huduma kwa wananchi .

Bodi ya ushauri ya hospitali ya rufaa ya Mkoa iliyopita ilimaliza muda wake **Tarehe 31 Julai, 2016**. Kuanzia kipindi hicho hospitali imekuwa ikijiendesha bila usimamizi wa bodi.

***Ndugu Wajumbe,***

Bodi hii teule imeteuliwa na Waziri mwenye dhamana na masuala ya Afya tangu tarehe 01 Machi, 2017 na itahudumu mpaka tarehe 31 Aprili, 2019. Nichukue fursa hii kuwapongeza sana wajumbe mlioteuliwa kwenye bodi hii mpya. ***Naomba mkafanye kazi kwa uaminifu mkubwa kama mlivyoaminiwa.***

Kazi kubwa ya bodi ni kuisimamia kwa karibu sana menejimenti ya hospitali ya rufaa ya Mkoa katika utekelezaji wa majukumu yake. Kimsingi menejimenti ya hospitali inawajibika moja kwa moja kwa bodi. Kiongozi wa menejimenti ya hospitali ni mganga mfawidhi wa hospitali ya rufaa ya Mkoa. Katika muundo wa bodi, mganga mfawidhi wa hospitali ya rufaa ya Mkoa  ni Katibu wa bodi ambaye anawajibika moja kwa moja katika utekelezaji wa majukumu na maazimio ya bodi. Yeye pia anawajibika katika utendaji wa kila siku wa shughuli za hospitali ya rufaa ya Mkoa. Kutofanya kazi kwa ufanisi kwa bodi hasa katika utekelezaji wa maazimio, kutakuwa kumechangiwa sana na utendaji wa katibu wa bodi ambaye pia ni Mganga mfawidhi wa Hospitali ya Mkoa kama nilivyosema. Hivyo, ni lazima kutengeneza mazingira mazuri ya mawasiliano na mazingira wezeshi ili kufanikisha utendaji madhubuti wa bodi hii.

***Ndugu Wajumbe,***

Bodi hii ni bodi ya ushauri, Kazi yake kubwa ni kuishauri menejimenti ya hospitali na mamlaka zingine kuwezesha utendaji kazi wa menejimenti na hospitali kutoa huduma bora kwa kufuata Miongozo, Sheria, Kanuni na Taratibu za Nchi. Serikali inahitaji bodi inayofanya kazi kwa ubunifu na kwa kujitolea. Sio bodi inayofanya kazi kwa kutegemea uwepo wa posho. Kuna baadhi ya wajumbe wa bodi wa awamu zilizopita walikuwa wanagoma kuja kwenye vikao mpaka fedha za kuwalipa posho zitakapopatikana. Wajumbe wa namna hiyo kama wapo kwenye bodi hii basi ni vema wabadilishe mitazamo yao. Bodi inapaswa kuisaidia hospitali ili iweze kupata fedha zitakazosaidia kuendesha hospitali na kuibua fursa mbalimbali zitakazoboresha upatikanaji wa huduma bora.

***Kwa kweli, Sisi upande wa Serikali hatutasita kuivunja bodi hii kama itashindwa kufanya kazi zake au itakuwa mzigo kwa hospitali kinyume na matarajio yetu.***

Bodi inajukumu la kupokea misaada yote ya kifedha au vitu vinayotolewa na wadau mbalimbali wa maendeleo na kusimamia matumizi ya misaada hiyo kupitia kwa katibu wa bodi. Katika suala hili pia inawajibu wa kutafuta misaada ya aina mbalimbali itakayosaidia kuendesha hospitali.

Bodi inatakiwa kukutana mara nne kwa mwaka, kila mwisho wa robo ya mwaka bodi inakutana na kupitia na kuidhinisha au kuikataa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya hospitali kabla ya kuiwasilisha kwenye timu ya usimamizi wa huduma za afya ya Mkoa (Regional Health Management Team) inayoongozwa na Katibu Tawala Msaidizi sehemu ya Afya (Mganga Mkuu wa Mkoa). Aidha, Bodi inaweza kukutana wakati wowote kwa dharura ili kuweza kushughulikia suala lolote la dharura lililojitokeza ambalo linaweza kuleta athari katika utoaji wa huduma au vyovyote ambavyo bodi itaona inafaa.

Bodi pia inajukumu kubwa la kupitia maombi yanayoletwa na menejimenti ya hospitali juu ya ubadilishwaji wa bei za uchangiaji huduma za afya. Kazi hii inapaswa kupitiwa kwa umakini na kushirikisha wadau mbalimbali ili wadau wote wa Sekta ya Afya wawe wameshirikishwa kikamilifu. Miongozo, Sheria, Kanuni na Taratibu lazima zipitiwe kwa kina. Baada ya kujiridhisha ndipo bodi inaridhia na kuwasilisha mapendekezo ya mabadiliko hayo kwa Waziri mwenye dhamana.

***Ndugu Wajumbe,***

Ikumbukwe kwamba wajumbe wa bodi wameteuliwa kwa kufuata vigezo mbalimbali, moja ya vigezo hivyo ni kuwa na uwakilishi mpana katika Halmashauri zote za Mkoa wa Shinyanga.

Katika hotuba ya Katibu Tawala Mkoa ameanisha taaluma mbalimbali za wajumbe wa bodi hii, baadhi ya taaluma hizo ni Biashara, Sheria, Udaktari, Ualimu nk. Wote kwa ujumla wenu tumieni taaluma zenu katika kuisaidia hospitali ili baadhi ya miradi inayoendeshwa na hospitali iweze kuleta faida ambayo itaongeza makusanyo ya fedha bila kuathiri huduma kwa wananchi. Bodi itasaidia kupitia miradi na mikataba mbalimbali ili kuona kama ina tija kwa taasisi.

***Ndugu Wajumbe,***

Kuna baadhi ya vigezo ambavyo vitasababisha ukomo wa mjumbe wa bodi, baadhi ya vigezo hivyo ni kama ifuatavyo:

1. Endapo mjumbe atahama kwenda Mkoa mwingine
2. Mjumbe akifariki
3. Mjumbe akiugua ugonjwa wa akili
4. Mjumbe akijiuzulu

Ikitokea hivyo, Waziri mwenye dhamana atapewa taarifa na atateua mjumbe mwingine kujaza nafasi itakayo achwa wazi.

***Ndugu wajumbe, Wageni waalikwa, mabibi na mabwana***

Kwa mara nyingine tena ninawapongeza sana wajumbe wote kwa kuchaguliwa kwenu kuwa wajumbe wa bodi hii mpya. Serikali ngazi ya Mkoa itawapa ushirikiano wa kutosha, kukiwa na suala lolote ambalo

mnafikiri linahitaji nguvu ya Serikali basi msisite kumuona Mganga Mkuu wa Mkoa, Katibu Tawala wa Mkoa au mimi mwenyewe.

***Baada ya kusema hayo, sasa natamka Rasmi kwamba BODI YA USHAURI YA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA imezinduliwa rasmi leo tarehe 17 Mei, 2017***

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza!!